TANGAZO LA SERIKALI Na.1003 La Tarehe 6/12/2024

SHERIA YA MISITU,

(SURA YA 323)

NOTISI

(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 29(1))

NOTISI YA KUSUDIO LA KUTANGAZA MABADILIKO YA ENEO LA MSITU WA HIFADHI WA TAIFA USINDAKWE YA MWAKA 2024

KWA KUWA, Eneo la Msitu wa Hifadhi wa Taifa Usindakwe lilitangazwa chini ya Tangazo la Serikali Namba 6 la Mwaka 1953 kuwa Eneo la Msitu wa Hifadhi wa Taifa Usindakwe;

KWA KUWA, Waziri, kwa mamlaka aliyopewa chini ya Sheria ya Misitu, Sura ya 323 anaona kwamba ni kwa maslahi ya umma kufanya mabadiliko ya eneo la Msitu wa Hifadhi wa Taifa Usindakwe;

NA KWA KUWA, Waziri, kwa kuzingatia Sheria ya Misitu ambayo, pamoja na masharti mengine inamtaka, anapokusudia kutangaza mabadiliko ya eneo la Msitu wa Hifadhi wa Taifa, kutoa notisi ya kusudio kwa umma kabla ya kutekeleza mamlaka hayo;

HIVYO BASI, Waziri anatamka kama ifuatavyo:

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Kusudio la Kutangaza Mabadiliko ya Eneo la Msitu wa Hifadhi wa Taifa Usindakwe ya Mwaka 2024.

Eneo linalopendekezwa kutangazwa

2. Eneo la hifadhi lililo ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Jedwali linapendekezwa kutangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Usindakwe.

Madhumuni ya tangazo

3. Madhumuni ya mabadiliko ya eneo la Msitu wa Hifadhi wa Taifa Usindakwe ni-

(a) kuondoa sehemu ya eneo la ardhi ya Msitu wa Hifadhi ya Taifa Usindakwe ili kutatua migogoro

ya; na

(b) kuhifadhi baioanuwai, vyanzo vya maji ili kuendeleza madhumuni ya usimamizi, uhifadhi wa eneo la msitu na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu katika eneo la msitu.

Uhalali wa Notisi

4.-(1) Notisi hii itakuwa halali kwa muda wa siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

(2) Ndani ya kipindi hicho cha siku tisini, mtu au kundi la watu au mwakilishi wao anaweza, kwa maandishi kuwasilisha pingamizi, maoni au madai ya haki yoyote inayotokana na sheria za kimila kuhusiana na ardhi au mazao ya msitu au haki yoyote iliyoainishwa kwenye sheria nyingine katika eneo la Msitu wa Hifadhi wa Taifa Usindakwe ambalo linapendekezwa kubadilishwa.

Uwasilishaji wa pingamizi

5. Pingamizi, maoni au madai yoyote dhidi ya kusudio la kutangaza mabadiliko ya eneo la Msitu wa Hifadhi wa Taifa Usindakwe yawasilishwe ndani ya siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa kwa Notisi hii kwa anuani ifuatayo:

Katibu Mkuu,
Wizara ya Maliasili na Utalii,
S.L.P. 1351,
DODOMA.

Tangazo la Serikali Na.1003 (Linaendelea.)

JEDWALI

(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)

WILAYA YA GEITA

MSITU WA HIFADHI WA USINDAKWE

Makadirio ya eneo: Hekta 290.2 au Kilometa za Mraba 2.90 Unakopatikana na Mipaka:

Eneo lote la hifadhi awali chini ya Eneo la Msitu wa Hifadhi wa Usindakwe linalopatikana Wilaya ya Geita, Mkoa wa Geita kama lilivyochorwa katika Ramani Na. Jb 3203 (Skeli 1:10,000) iliyohifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Idara ya Upimaji na Ramani na lenye mipaka ifuatayo:



Dodoma,
12 Novemba, 2024

PINDI HAZARA CHANA,
Waziri wa Maliasili na Utalii